

## **JIHADHARI NA UTAPELI KUHUSU HUNDI ZA MSAADA WA KICHOCHEO KIKOSI DHIDI YA UTAPELI. ABQ**

Bunge limeidhinisha msaada kutoka kwa serikali kuu ili kusaidia idadi kubwa ya wananchi, kupunguza makali ya upotevu wa mapato kutokana na dharura ya ugonjwa wa Covid-19. Hundi zitatumwa baada ya majuma machache. Hii ina maana ya kwamba hundi yako itaingizwa kwenye akaunti ya benki yako (kama taarifa hizo zipo katika mapato yako ya kodi uliyojaza awali) au hundi itatumwa kwako kwa njia ya posta.

Matapeli tayari wanajaribu kuchukua fursa hii kujinufaisha.

**Jinsi ya kung'amua utapeli kuhusiana na "kichochezi" cha Serikali kuu dhidi ya Covid-19:**

- **Mwakala wa serikali hawatawasiliana nawe kupitia vyombo vya habari vya kijamii, simu, ujumbe wa maandishi au barua pepe.**
- **Mwakala wa serikali hawatakuuliza uthibitisho habari zako binafsi au kutoa maelezo ya benki. Sio "lazima" kutoa habari hii ili kupokea hundi yako ya uhamasishaji.**
- **Mwakala wa serikali hawatauliza nambari yako ya soshu.**
- **Mwakala wa serikali hawatawasiliana nawe ili upate pesa zako "mara moja" au "haraka".**
- **Mwakala wa serikali hawatakuuliza ulipe "ada ya mchakato".**

Ikiwa tapeli atakuita au kuwasiliana nawe, usiongee naye, zima simu - futa barua pepe- usiifungue.

### **KUWA MWANGALIFU:**

- **Wajifanyao kuwa ni serikali** - tofautisha tovuti za kweli na tovuti za bandia. Hakikisha ni tovuti halali ya serikali kabla ya kuamini habari yoyote unayopewa.
- **Unapokuwa na shaka**, chukulia kama ni utapeli.

Tovuti za serikali: IRS: [www.irs.gov/coronavirus](http://www.irs.gov/coronavirus).  
US Treasury: <https://home.treasury.gov/>

TOA TAARIFA ZA UTAPELI KWA: Federal Trade Commission: <https://www.ftc.gov/>

[www.cabq.gov/scams](http://www.cabq.gov/scams) Au Piga 311 kwa msaada  
ALBUQUERQUE CONSUMER FINANCIAL PROTECTION INITIATIVE